**USHIRIKIANO** | Miongoni mwa mafanikio ambayo nchi hiyo ya Asia Mashariki inajivunia kuleta Kenya ni kujenga mabwawa na kustawisha kilimo cha mchele

# Japani kuadhimisha miaka 60 ya ushirikiano na Kenya Januari

**Sherehe za kufurahia kipindi hicho kirefu cha ushirikiano zitafanyika katika vyuo vikuu na taasisi nyinginezo nchini**

**NA MWANDISHI WETU**

HIVI majuzi katika mechi za Kombe la Dunia zilizokamilika jana nchini Qatar, ipo timu iliyoshangaza ulimwengu kwa kuwa timu pekee iliyoamua kuusafisha uwanja waliouchezea mbali na kuvinadhifisha vyumba vyao kabla ya kuenda uwanjani kwa michuano.

Timu hiyo si nyingine ila Japani. Lakini yamkini usilolijua ni kuwa hiyo ni sifa moja tu kati ya nyingi za raia wa taifa hilo lenye visiwa vingi linalopatikana barani Asia ya Mashariki.

Mbali na usafi wa kupigiwa mifano, Wajapani wanajulikana sana kwa ubunifu wa kuajabisha, ni wapenda utamaduni wao, wastaarabu, na wenye bidii ya mchwa.

Si siri kuwa Wajapani ni wachapa kazi kiasi cha kusahau likizo zao mara kwa mara hata baada ya kupokezwa marupurupu ya likizo hizo.

Kuna wakati ambapo madereva wa Japani walishiriki mgomo lakini waliendelea kuendesha mabasi ila tu hawakulipisha abiria nauli.

Kenya inatarajiwa kunufaika kutokana na ubunifu wa nchi hiyo inayojulikana sana katika masuala ya kiteknolojia.

Wala si kwamba Japani imeanza kushirikiana na Kenya leo au jana; imekuwa ikishirikiana na Kenya kwa miaka 60 sasa. Ushirikiano huu umechangia maendeleo ya kiteknolojia, kiviwanda, kilimo, kiafya, nishati, misitu, elimu, mazingira, huduma za maji na ujenzi.

Baadhi ya miradi ambayo imefanikishwa nchini ni kama vile mradi wa kawi wa Sondu Miriu, Kengen, Kemri, Chuo cha JKUAT, na madaraja mbalimbali Pwani. Miradi hii imefanywa kupitia Shirika la Kijapani (JICA).

Sherehe za kuadhimisha miaka 60 ya ushirikiano baina ya nchi hizi mbili itaaandaliwa kuanzia Januari mwaka ujao.

"Tumeandaa miradi mingi ya kuadhimisha ndoa yetu na Kenya. Ndoa ambayo imekuwa na amani na upendo bila misukosuko," asema naibu wa Balozi wa Japani nchini Kenya, Kitagawa Yahusiha.

Aliongeza kuwa maadhimisho haya yataibua mwanzo mpya katika ushirikiano huu wa kidiplomasia na kiuchumi.

Katika kilimo, Japani imezingatia sana upanuzi wa kilimo cha mpunga kupitia unyunyiziaji maji na kuongeza kiwango cha uzalishaji wa mchele hadi tani 200,000 mbali na kuchangia katika kubuni nafasi za kazi katika maeneo ya nyanjani hasa katika eneo la Mwea, Kaunti ya Kirinyaga na Ahero katika Kaunti ya Kisumu.

Ingawa kumekuwa na misukosuko iliyochangia kuchelewa kwa baadhi ya miradi inayodhaminiwa na Japani, kuna matumaini kwamba sherehe hizi zitatia moyo wadau ili wajitahidi zaidi kufanikisha maendeleo.

Kwa mfano, ujenzi wa Bwawa la Thiba (ambao sasa ni afueni kuu kwa wakulima wa Mwea) uliokamilika miezi michache iliyopita na kufunguliwa rasmi na Rais William Ruto, ulichukua zaidi ya miaka 20 kukamilika kwa sababu ya hasa wenyeji kukataa ardhi yao ichukuliwe.

Wakulima wa Mwea wanatarajia kwamba ushirikiano huu hautakoma bali utazidi kuleta mabadiliko katika maisha yao.

Kupitia shirika la JICAambalo hutekeleza maendeleo kwa niaba ya serikali ya Japani- na kwa ushurikiano na Bodi ya Unyunyiziaji Maji (National Irrigation Board) takribani Sh13 bilioni zimetumika katika ujenzi wa Bwawa la Thiba ambalo linasambaza maji kwa umbali wa kilomita 14 kwenye mashamba ya mpunga Mwea.



Mashine ya Combined Harvester katika shamba la mpunga Mwea, Kaunti ya Kirinyaga. PICHA|HISANI



Naibu Balozi wa Japani Kenya, Kitagawa Yahusiha katika shamba la mpunga Mwea, Kirinyaga.

Kabla Bwawa hili kujengwa, wakulima walikuwa wakipata mazao machache sana ya mchele. Hata hivyo, sasa wanapata karibu tani milioni mbili.

Pia wamefaidikia kwa mashine sita za kuvuna mchele ambazo zimerahisishaji shughuli ya uvunaji kutoka saa 10 hadi dakika 45 pekee.

"Sisi kama wakulima tangu Wajapani watunjengee bwawa na kutuma mitambo ya kuvuna mchele kwa kasi, tumeongeza kiwango tunachovuna na tuna matumaini kwamba wanapoadhimisha miaka 60 ya ushirikiano na Kenya, hawatatuacha."

Jambo moja ambalo ningependa kusisitiza ni kwamba Wakenya wengi bado hawafahamu umuhimu wa mchele kama chakula," asema Paul Njuguna, mkulima wa mpunga Mwea.

"Katika ushirikiano wetu, lengo letu ni kuongeza maarifa ya Wakenya kisha baadaye kusambazia maarifa watu wengine. Kuna wataalamu mbalimbali wa Kenya ambao washapata ujuzi wa kilimo, teknolojia, afya na uhandisi na sasa wanawafunza watu wengine," hiyo ndiyo furaha yetu kwani njia mojawapo ya kuonyesha upendo ni 'kusambaza maarifa," aongeza Balozi Kitagawa.

Umuhimu wa mchele unazidi kupewa umuhimu hasa kutokana na ripoti kwamba mchele unazidi kuliwa kwa kiwango zaidi ya maradufu nchini Kenya ukilinganisha na vyakula vingine na katika sherehe hizi, Wakenya watukuwa wakisubiri kwa hamu kusikia iwapo Japani itatangaza maendeleo mapya na pia kuimarisha nguvu zao ka kimaendeleo katika vizazi vijavyo.

Kuanzia mwezi ujao, kutakuwa na makongamano kwenye vyuo vikuu na warsha mbalimbali kuadhamisha ushirikiano huu na kupiga darubini uwezekano wa kuendeleza ushirikiano huu katika kipindi kijacho